

Tamko la Makubaliano:
Mapitio ya Uthibitisho
Statement of Understanding: Mid-Certification Review



Ili kuendelea kupata fedha taslimu au usaidizi wa chakula, ni lazima ujaze fomu ya Mapitio ya Uthibitisho. Kuna njia tatu za wewe kujaza haya mapitio yako:

1. Kwa simu kwa kupiga 1-877-501-2233.
2. Kwa kujaza fomu DSHS 14-467 na
 - Kuituma kama nukushi kwetu kupitia 1-888-338-7410; au
 - Kuituma kwa njia ya posta kupitia PO BOX 11699, TACOMA WA 98411.
3. Kwa kujadili mazingira yako pamoja nasi katika ofisi mahalia, kusaini na kuandika tarehe kwenye fomu hii.

Nini unalazimika kukiripoti kwenye Mapitio ya Uthibitisho:

- Badiliko la anwani na gharama za makazi yako kwenye anwani mpya.
- Mabadiliko ya aishiye kwenye kaya yako.
- Mabadiliko ya kipato chako kutoka **chanzo chochote**. Hii inajumuisha kipato kutokana na kufanya kazi, fidia ya kutoajiriwa, huduma za kijamii, Kazi na Viwanda, na matunzo ya watoto.
- Mabadiliko ya matunzo yoyote ya watoto ambayo unatakiwa kisheria kuyalipa kwa ajili ya mtoto usiyeishi naye.
- Kama huna watoto kwenye kaya yako, na saa za kazi za mtu anayejiweza zimeshuka chini ya saa 20 kwa wiki.

Soma kwa umakini na saini kabla ya kurudisha fomu hii:

- Naelewa kwamba kanuni za DSHS zinanihitaji nijaze fomu ya mapitio ya Uthibitisho na niwaambie DSHS kuhusu mabadiliko ya mazingira katika kaya yangu kulingana na WAC 388-418-0005 na WAC 388-418-0011.
- Naelewa kwamba ni kosa la jinai kwangu kusema uongo ili kupata fedha taslimu au mafao ya chakula. Naelewa pia kwamba ni kosa la jinai kama nisipowaambia DSHS jambo ambalo najua napaswa kuliripoti.
- Naelewa kwamba kama nitatoa taarifa ninayofahamu kuwa ni uongo, naweza kushitakiwa kwa kosa la jinai.
- Naelewa adhabu za kuvunja kanuni za usaidizi wa chakula zinajumuisha kuondolewa sifa ya kupata usaidizi wa chakula, faini, au kifungo cha gerezani.
- Naelewa kwamba kama nisipotoa uthibitisho wa mabadiliko ambayo yanaweza kufanya mafao yangu yaongezeke, DSHS haitatumia mabadiliko haya kubaini mafao yangu.
- Naelewa kwamba kile nilichowaambia idara husika katika ripoti hii kinaweza kuathiri mafao yangu.
- Natamka chini ya adhabu ya kiapo cha uongo kuwa taarifa niliyowapa DSHS katika ripoti hii ni ya kweli na sahihi kadri ya uelewa wangu.

SAINI	TAREHE	ANDIKA JINA	NAMBARI YA UTAMBULISHO WA MTEJA

